


# Kisasi cha Kiongozi

La revanche de l'indicateur



✎ Zulu folktales  
👤 Wiehan de Jager  
📖 Brigid Simiyu  
🗣️ Kiswahili / French  
📊 Level 4

# Storybooks Canada

[storybookscanada.ca](http://storybookscanada.ca)

Kisasi cha Kiongozi / La revanche de  
l'indicateur

Written by: Zulu folktales

Illustrated by: Wiehan de Jager

Translated by: (sw) Brigid Simiyu, (fr) Alexandra

Danahy

This story originates from the African Storybook  
([africanstorybook.org](http://africanstorybook.org)) and is brought to you by  
Storybooks Canada in an effort to provide  
children's stories in Canada's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons

[Attribution 3.0 International License](https://creativecommons.org/licenses/by/3.0).

<https://creativecommons.org/licenses/by/3.0>



Hii ni hadithi ya Ngede, Kiongozi, na mvulana mmoja mlafi anayeitwa Gingile. Siku moja Gingile alipokuwa akiwinda alisikia mwito wa Ngede. Kinywa chake kilianza kutokwa mate kwa kufikiria juu ya asali. Alisimama, akasiliza na kuangalia vizuri hadi alipomwona yule ndege akiwa ametua kwenye matawi yaliyokuwa juu ya kichwa chake. “Chitik-chitik-chitik,” yule ndege mdogo alitatarika aliporuka na kutua kwenye mti uliokuwa karibu, tena na mwingine. “Chitik-chitik-chitik,” aliita, huku akinyamaza na kuhakikisha kwamba Gingile alikuwa amemfuata.

...

Voici l’histoire de Ngede l’indicateur et un jeune homme avide nommé Gingile. Un jour, lorsqu’il chassait, Gingile entendit l’appel de Ngede. Gingile commença à saliver en pensant au miel. Il arrêta et écouta attentivement, fouillant jusqu’à ce qu’il trouve l’oiseau dans les branches au-dessus de sa tête. « Chitik-chitik-chitik, » le petit oiseau ébranla, en volant d’un arbre à l’autre. « Chitik-chitik-chitik, » il lança, arrêtant de temps en temps pour s’assurer que Gingile le suivait.

Après une heure et demie, ils atteignirent un figuier sauvage énorme. Ngede sautilla éperdument parmi les branches. Il s'installa ensuite sur une branche et inclina sa tête vers Gingile comme pour dire, « Le voici ! Viens vite ! Qu'est-ce qui te prend autant de temps ? » Gingile ne pouvait pas voir d'abeilles du dessous de l'arbre, mais il avait confiance en Ngede.

...

Baada ya nusu saa, walifikia mti wa mtini. Ngede aliruka kama mwenda wazimu kutoka tawi moja hadi jingine. Kisha alitulia kwenye tawi moja na kupindua kichwa chake kumwambia Gingile kama kusema, "Iko hapa! Njoo sasa! Kwa nini unachukua muda mrefu?" Gingile hakuweza kuona nyuki wowote kutoka chini ya mti, lakini alimwamini Ngede.






Kwa hivyo Gingile aliweka mkuki wake alioutumia kuwinda chini ya mti, akakusanya vijiti vilivyokauka na kuwasha moto mdogo. Moto ulipokuwa ukiwaka vizuri, aliweka kijiti kirefu katika mwake. Mti huu ulijulikana kwa kutoa moshi mwingi ulipochomeka. Alianza kukwea mti huku akishika kwa meno yake sehemu isiyomeka.

...

Alors, Gingile dépossa sa lance sous l'arbre, recueilli des brindilles séchées et alluma un petit feu. Un coup que le feu brûlait bien, il mit une longue branche au cœur du feu. Ce bois était connu pour la fumée qu'il créait quand il brûlait. Gingile commença à grimper, tenant entre ses dents le bout froid de la branche qui fumait.



Muda mfupi baadaye, aliweza kusikia sauti ya nyuki wakijiibidisha. Walikuwa wakilingia na kutoka kwenye upenyo wa mti, yaani mzinga wao. Gingile alipoufikia mzinga, alisukuma ile kuni ya moto ndani ya ule upenyo. Nyuki waliharakisha kutoka ndani wakiva na hasira na uchungu. Waliruka na kwenda mbali kwa sababu hakupenda moshi – lakini walifanya hivyo baada ya kumuuma Gingile kwa uchungu!

...

Bientôt il pouvait entendre le bourdonnement bruyant des abeilles chargées. Elles rentraient et sortaient d'un creux dans le tronc d'arbre - leur ruche. Lorsque Gingile rejoint la ruche il mit le bout fumant de la branche dans le creux. Les abeilles sortirent, fâchées et méchantes. Elles s'envolèrent parce qu'elles n'aimaient pas la fumée - mais pas avant d'avoir donné des piqûres douloureuses à Gingile !



Kwa hivyo wakati watoto wa Gingile wanaposikia hadithi ya Ngede, wanamheshimu yule ndege. Kila wanapotoa asali, huhakikisha kwamba wanamwacha kiongozi fungu kubwa!

...

Ainsi, quand les enfants de Gingile entendent l'histoire de Ngede ils respectent le petit oiseau. Chaque fois qu'ils récoltent du miel, ils s'assurent de laisser la plus grande partie du rayon pour l'indicateur !



Nyuki walipokuwa nje, Gingile aliingiza mikono yake ndani ya kiota. Alitoa kipande kikubwa cha sega kilichokuwa kinadondoka urojo mwingi wa asali nyeupe. Aliiweka taratibu ndani ya mkoba aliokuwa nao na kuanza kushuka kutoka mtini.

...

Quand les abeilles furent sorties, Gingile enfonça ses mains dans le nid. Il sortit des poignées du nid desquelles s'écoulaient du miel riche et des larves grasses et blanches. Il mit le nid soigneusement dans la besace il portait sur son épaule et commença à descendre de l'arbre.



Kabla ya Chui kumvamia Gingile, alishuka chini haraka. Katika haraka hiyo, aliteleza na kuanguka kwa kishindo huku akiumia mguu wake. Alirukaruka akienda kwa haraka alivyoweza. Kwa bahati nzuri, Chui alikuwa bado amelala kwa hivyo hakumfukuza. Ngede, Kiongozi alikuwa amelipiza kisasi chake na Gingile alikuwa amejifunza funzo lake.

...


Avant que Léopard puisse s'en prendre à Gingile, ce dernier se précipita en bas de l'arbre. Dans son empressement, il manqua une branche et atterrit par terre avec un bruit sourd, tordant sa cheville. Heureusement pour lui, Léopard était encore trop endormi pour le poursuivre. Ngede, l'indicateur, eu sa revanche. Et Gingile retint sa leçon.



Ngede alishuhudia kila kitu Gingile alichofanya. Alikuwa anamsubiri abakishhe kiasi kidogo cha asali kama shukurani kwa kiongozi. Ngede aliruka kutoka tawi hadi tawi huku akikaribia chini. Mwishowe Gingile alifika chini ya mti. Ngede alitua kwenye mwamba karibu na mvulana huyo na kusubiri zawadi yake.

...

Ngede regardait avec impatience tout ce que Gingile faisait. Il attendait qu'il laisse un gros morceau de nid d'abeille comme signe de remerciement pour l'indicateur. Ngede voltigeait de branche en branche, de plus en plus près du sol. Finalement, Gingile arriva au pied de l'arbre. Ngede se percha sur une roche près du garçon et attendit sa récompense.



Gingile alipopanda, alishangaa kwa nini hakusikia sauti ya nyuki. "Pengine mzinga umo ndani zaidi katika mti," alifikiria. Alipanda tena juu ya tawi jingine. Lakini badala ya mzinga, alikuwa alijikuta amekodolewa macho na Chui! Chui alikuwa na hasira sana kwa sababu usingizi wake ulikuwa umekatizwa. Aliyafanya macho yake kuwa madogo, akautungua mdomo wake na kuonyesha meno yake makubwa na makali.

...

Gingile grimpa, se demandant pourquoi il n'entendait pas le bourdonnement habituel. « Peut-être que la roche est très profonde dans l'arbre, » se dit-il. Il se remonta sur une autre branche. Mais au lieu de la roche, il arriva face-à-face avec le visage d'un léopard ! Léopard était très fâché que son sommeil ait été interrompu si brusquement. Elle plissa ses yeux et ouvrit sa bouche pour révéler ses grandes dents pointues.



Lakini Gingile alizima moto, akachukua mkuki wake na kuanza safari kwenda nyumbani bila kumjali ndege yule. Ngede aliita kwa hasira, “USH-ndi! USH-ndi!” Gingile alisimama, akamkodolea macho yule ndege kisha akacheka kwa sauti. “Unataka asali kidogo, rafiki yangu? Ha! Lakini ni mimi niliyefanya kazi yote pamoja na kuumwa na nyuki. Kwa nini nikugawie hii asali tamu?” Baada ya kusema hivyo, aliondoka na kwenda zake. Ngede alikasirika sana! Hivi sivyo alivyostahili kutendewa! Ila atalipiza kisasi.

...

Mais Gingile éteint le feu, ramassa sa lance et commença à rentrer chez lui, en ignorant l’oiseau. Ngede lança, fâché, « VIC-torr ! VIC-torr ! » Gingile arrêta, dévisagea le petit oiseau et éclata de rire. « Tu veux du miel, mon ami ? Ha ! Mais c’est moi qui ai fait tout le travail et reçu toutes les piqûres. Pourquoi est-ce que je devrais partager ce miel avec toi ? » Et il quitta. Ngede était furieux ! Cela n’était aucune manière de le traiter ! Mais il aurait sa revanche.



Siku moja baada ya majuma machache, Gingile tena alisikia mwito wa asali kutoka kwa Ngede. Aliikumbuka asali tamu, na kwa hamu alimfuata ndege yule kwa mara nyingine. Baada ya kumwongoza Gingile pembeni mwa msitu, Ngede alisimama na kupumzika chini ya mti wa mwavuli. “Ahh,” Gingile aliwaza. “Lazima mzinga umo ndani ya mti huu.” Kwa haraka aliwasha moto wake na kuanza kukwea mti huku akibeba kuni iliyotoa moshi katika meno yake. Ngede alikaa na kuangalia tu.

...

Un jour, plusieurs semaines plus tard, Gingile entendit de nouveau l’appel de Ngede. Il se souvint du miel délicieux et suivi avec impatience l’oiseau une fois de plus. Après avoir mené Gingile le long de la forêt, Ngede arrêta pour se reposer dans un acacia faux-gommier. « Ahh, » pensa Gingile. « La ruche doit être dans cet arbre. » Il parti rapidement son petit feu et commença à grimper, la branche fumante entre ses dents. Ngede, assis, le regardait.